# KANUNI ZA KILIMO BORA CHA ZAO LA UFUTA

## 1.0 Utangulizi

Ufuta ni zao aina ya mbegu za mafuta ambalo hutumika kama zao la chakula na pia zao la biashara. Mbegu zake hutoa mafuta bora yasiyokuwa na lehemu. Pia hutumika kutengeneza vyakula mbalimbali kama vile kashata na tui, vilevile huchanganywa katika mikate, unga wa lishe na siagi. Baada ya kukamua mafuta, mashudu yake hutumika kulisha mifugo. Tanzania ufuta hustawi mikoa mingi, baadhi ya mikoa hiyo ni Lindi, Mtwara, Ruvuma, Pwani, Dodoma, Manyara, Songwe, Morogoro, Singida, Katavi na Mbeya. Kilimo bora cha ufuta ni chachu ya uzalishaji wenye tija. Humhakikishia mkulima kupata mavuno mengi yenye tija na ubora unaotakiwa na soko pamoja na walaji. Zifuatazo ni kanuni za kilimo bora cha ufuta.

## 2.0 Mazingira ya Ustawishaji

Ufuta hustawi vizuri katika maeneo yenye mwinuko wa mita 0-1500 kutoka usawa wa bahari. Huhitaji mvua ya wastani wa milimita 400 hadi 800 kwa mwaka. Hustawi vizuri kwenye udongo tifutifu wenye rutuba na usiotuamisha maji. pH ya udongo iwe 5.5-8.0.

## 3.0 Utayarishaji wa Shamba

Shamba litayarishwe mapema kabla ya kupanda. Utayarishaji wa shamba unahusisha kuondoa visiki (kwa shamba jipya) na kutifua kwa trekta, jembe la mkono au la kukokotwa na wanyama.



*Utayarishaji wa shamba*

## 4.0 Kutumia mbegu bora

Hakikisha unapata mbegu bora zinazozalishwa na TARI-Naliendele au wakala wa mbegu za Kilimo (ASA) au kutoka makampuni/taasisi zinazotambulika kisheria. Mbegu bora za ufuta huzaa vizuri na huvumilia mashambulizi ya magonjwa na wadudu. Mbegu hizo ni Lindi 02, Ziada 94, Mtondo 13, Naliendele 92, Mtwara 09 na Zawadi 94. Kiasi cha mbegu kinachohitajika kwa ekari moja ni kilo 1-1.5

## 5.0 Upandaji

Baada ya uandaaji wa shamba na mbegu kukamilika, hatua inayofuata ni upandaji. Upandaji ufanyike kutegemeana na msimu wa mvua. Kwa mfano kanda ya kusini upandaji unaweza kuanza mwishoni mwa mwezi Disemba hadi katikati ya mwezi Februari. Mbegu bora nyingi hukomaa ndani ya siku 100-130 hivyo upandaji ulenge kipindi cha msimu wa mvua ili kuepuka mazao kukomaa na kuvunwa wakati mvua zinaendelea kunyesha. Ufuta ukikomaa na kuvunwa kipindi mvua ya msimu inaendelea kunyesha hupunguza ubora wa ufuta. Mkulima apande ufuta kwa mstari, nafasi kati ya mstari mmoja hadi mwingine sentimita 50 na mche hadi mche ni sentimita 10. Kwa vile ufuta hupandwa kwenye mifereji ya kina cha sentimita 2-3, nafasi ya mche na mche hupatikana kipindi cha kupunguzia miche. Ili kuhakikisha mtawanyiko mzuri wa mbegu kwenye mfereji mkulima anashauriwa kuchanganya mbegu na mchanga katika uwiano wa kilo 1 ya mbegu kwa debe 4 za mchanga.



*Muonekano wa shamba la ufuta lililopandwa kwa mistari*

## 6.0 Palizi na upunguziaji ufuta

Ili kupata mavuno mengi na bora, mkulima anashauriwa kufanya palizi angalau mara tatu kwa msimu. Palizi inaweza kufanyika kwa kutumia jembe la mkono au viuagugu. Upunguziaji wa miche ufanyike baada ya wiki mbili tangu mbegu za ufuta kuota, kwa kuacha umbali wa sentimita 10 mche hadi mche.



*Shamba la ufuta uliopunguziwa*

## 7.0 Matumizi ya mbolea

Kama ilivyo mazao mengine ufuta nao unahitaji rutuba ya kutosha. Kama shamba halina rutuba ya kutosha inashauriwa kutumia mbolea za kupandia na kukuzia. Mfano wa mbolea za kupandia ni NPK,

DAP na TSP. Mbolea za kukuzia mfano Urea na SA. Mfuko mmoja wa kilo 50 za mbolea unatosha kwa ekari moja. Mbolea za samadi na mboji zitumike wakati wa kuandaa shamba.

## 8.0 Kudhibiti visumbufu vya ufuta

Zao la ufuta hushambuliwa na wadudu waharibifu na magonjwa mbalimbali. Wadudu waharibifu ni vibaruti, konokono na funza wa majani na vitumba. Magonjwa ya ufuta ni madoa ya majani, kuoza shina, ukoma wa majani ya ufuta na failodi. Kudhibiti visumbufu hivi, mkulima atumie mbegu bora, usafi wa shamba, kilimo cha mzunguko pamoja na kutumia viatilifu pendekezwa na kwa usahihi.

## 9.0 Uvunaji, Ukaushaji na kuhifadhi

Ufuta ukikomaa mashina hubadilika rangi toka kijani kuwa njano au kahawia na hupukutisha majani. Kwa kipindi hicho mkulima anashauriwa kuanza kuvuna, kufunga katika vitita na kuukausha katika chanja. Ufuta hukauka baada ya siku 14-21 kutegemea hali ya hewa. Baada ya kukauka inamishia vitita katika turubai, kitambaa safi, jamvi au sakafu huku ukipigapiga taratibu. Pepeta kuondoa takataka ili kupata ufuta safi. Weka ufuta safi katika mifuko (viroba) na kuhifadhi sehemu inayopitisha hewa ndani ya nyumba au ghala kwa kupanga juu ya chaga.



*Namna bora ya ukaushaji wa ufuta baada ya kuvuna*



*Namna ya kuhifadhi ufuta*

# KANUNI ZA KILIMO BORA CHA ZAO LA UFUTA



*Kimetayarishwa na:*

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania
TARI - Naliendele
S. L. P. 509
MTWARA
Email: cdnaliendele@tari.go.tz

**Mei 2022**